Taarifa kwa vyombo vya habari | 11 Machi 2020

Ndoa za Utotoni Hupunguza Ubora wa Maisha kwa Wasichana wadogo na Watoto wao, na Kuathiri Vibaya Uchumi wa Taifa kwa Ujumla

Vijana wawili wanaharakati wa kiume kupitia filamu yao wanapinga mitazamo na kutokuchukua hatua za kukomesha tatizo la ndoa za utotoni

11 Machi, Dar es salaam: Katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani 2020, vijana wawili wanaharakati wa kitanzania wamezindua filamu yao kuhusu ndoa za utotoni kwa kushirikiana na *Msichana Initiative* na *Twaweza*. Elias Maeda na Festo Henry Msangawale ni watetezi wa haki za kijinsia ambao wanalenga kufikisha ujumbe kwa jamii na viongozi wote nchini kuchukua hatua kuwasaidia wasichana wa umri mdogo kutimiza ndoto zao kwa kukomesha ndoa za utotoni.

Ingawa sheria inawalinda wasichana wadogo shuleni dhidi ya kuolewa na kukatisha masomo kupitia Sheria ya Elimu, Sheria ya Ndoa inaruhusu wasichana kuolewa wakiwa chini ya umri wa miaka 18. Hii inamaanisha kuwa wasichana walio nje ya mfumo wa shule, tayari wako hatarini zaidi kutolindwa na sheria. Hivi sasa, kuna amri ya Mahakama inayotaka Sheria ya Ndoa pia ibadilishwe ili kuwalinda wasichana wote wa umri mdogo. lakini amri hii bado halijatekelezwa.

Nchini Tanzania, wasichana 2 kati ya 5 wameolewa kabla ya kutimiza umri wa miaka 18. Nchi inaweza kuwa inapoteza kiasi cha Tsh milioni 637 kila mwaka (ilikadiriwa, 2015) mapato yanayopotea kwasababu ya ndoa za utotoni. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa 1% tu ya wasichana wadogo wenye umri wa miaka 15 hadi 19 ambao wameolewa wapo shuleni, ikilinganishwa na 45% ya wavulana wa umri huo huo ambao hawajaoa. Takwimu zinaonesha zaidi kuwa akina mama wenye elimu wanahakikisha watoto wao wana afya bora kuliko wenzao wasio na elimu.

- 41% ya wanawake wasio na elimu rasmi hujifungua katika vituo vya afya ikilinganishwa na 89% ya wenzao waliosoma kwa kiwango cha sekondari au zaidi
- Wanawake wasio na elimu rasmi wana uwezekano mdogo (38%) kuliko wale walio na elimu ya sekondari au zaidi (64%) kuwahi kutafuta matibabu kwa mtoto aliye na homa ndani ya siku moja
- Watoto wa akina mama wasio na elimu rasmi wana uwezekano mkubwa zaidi wa kupimwa na kukutwa na malaria, 21%, kuliko wale ambao mama zao wana elimu ya sekondari au ya juu (4%).

Filamu fupi iliyotengenezwa na wanaharakati vijana, Elias Maeda na Festo Msangawale, inagusa masuala yote ya msingi ya ndoa za utotoni. Katika filamu hiyo, inayoitwa Hellena, wazazi wanasukumwa na shauku yao ya kumwozesha binti yao. Ndoa za utotoni huathiri vibaya familia masikini: wanawake kutoka kaya masikini wana uwezekano mkubwa wa kuolewa wakiwa watoto (46%) ikilinganishwa na wenzao kutoka familia tajiri (16% waliolewa wakiwa bado ni watoto). Wanawake wa vijijini pia wana uwezekano mkubwa kuliko wanawake wa mijini kuolewa kabla ya kutimiza umri wa miaka 18 (37% dhidi ya 21%).

Wasichana wakiolewa wakiwa watoto wana fursa ndogo sana ya kupata elimu. Kati ya wasichana wenye umri wa miaka 15 hadi 19 ambao wameolewa, ni 1% tu wapo shuleni ikilinganishwa na 45% ya wasichana wa umri huo ambao hawajaolewa. Na hiki ndicho anakijutia sana Hellena kuhusu hali yake kwenye filamu - anataka kumaliza masomo yake na kuwasaidia wazazi wake siku zijazo.

Vivyo hivyo, 60% ya wanawake ambao waliolewa wakiwa watoto wanafanya kazi kwenye kilimo (wakulima) ukilinganisha na 39% ya wanawake ambao waliolewa wakiwa na umri wa miaka 20 au zaidi. Wanawake ambao

wameolewa wakiwa na miaka 20 au zaidi wana uwezekano mkubwa (14%) kuwa na kazi za kitaalam au ujuzi kuliko wenzao walioolewa wakiwa watoto (3%). Kwenye filamu hiyo, tunaona Hellena akijitahidi kutimiza majukumu yake mapya katika kazi ya kilimo ingawa alikuwa na ndoto ya kuwa rubani wa ndege.

Pia wasichana wadogo ambao wameolewa wakiwa watoto wanasumbuliwa sana na masuala ya kisaikolojia. Wanawake ambao wameolewa mapema wana uwezekano mkubwa wa kusema ni sawa kwa mume kumpiga mkewe ikiwa atatoka bila kumwambia (47%) ikilinganishwa na wale ambao waliolewa wakiwa na umri wa miaka 20 au zaidi (37%). Pia wana mamlaka/nguvu ndogo ya kufanya maamuzi katika nyumba zao, hasa juu ya fedha. Aidha, wake wenye umri mdogo (watoto) wana uwezekano mkubwa wa kukumbana na ukatili wa kimwili na kingono kuliko wenzao walioolewa wakiwa na umri mkubwa.

"Tulitaka kuongea na jamii, kuzifanya hadithi za dada zetu wadogo, marafiki zetu, ambao wanateseka sana kwa kulazimishwa kuolewa wakiwa wadogo, zisikike kwa umma," alisema Festo Henry Msangawale. *"Tunataka kila mtu atambue na aguswe na yanayowakuta mabinti zetu wenye umri mdogo ili sote tuchukue hatua sasa kumaliza ndoa za utotoni."*

Elias Maeda, mtayarishaji mwenza wa Hellena, alielezea maneno yake*.alisema "Tunajua kuwa mara nyingi kaya masikini zinapata ugumu mkubwa kufanya maamuzi kutokana na umasikini. Hawawezi kumudu gharama za kuelimisha na kuwasaidia watoto wao, na hivyo kuwaoza wasichana wao inaonekana ndio njia pekee. Lakini mara nyingi uamuzi huu husababisha matokeo mabaya zaidi. Kwa kuonesha mtiririko wa hadithi hii, tunatarajia kubadilisha maisha ya mamilioni ya wasichana wenye umri mdogo*

"Takwimu zinajieleza zenyewe," alisema Aidan Eyakuze, Mkurugenzi Mtendaji wa Twaweza. *"Ni mara chache sana kuona uhusiano wa wazi kama huu katika takwimu: ndoa za utotoni husababisha madhara kiafya na kimaisha kwa msichana mdogo na kwa watoto atakaowazaa baadaye, pamoja na kusababisha hasara kubwa kiuchumi kwa jamii na nchi nzima"*

"Mahakama hapa nchini imeshafanya maamuzi ya wazi kabisa kupinga ndoa za wasichana wenye umri mdogo," alisema Rebeca Gyumi wa Msichana Initiative. *"Bado tunajua kuwa katika jamii zetu nchini kote wasichana wenye umri mdogo wanaendelea kuteseka. Ndoa za utotoni zinachochea tofauti za mamlaka kwenye mahusiano, maslahi ya wanandoa na mashirikiano kijamii ambapo kwa miaka mingi wanawake na wasichana wamekuwa wahanga wa uonevu na dhuluma ndani ya jamii zetu. Ili kukomesha ndoa za utotoni ni lazima tuachane na tamaduni za kijinsia tulizozizoea na tusisitize uwajibikaji kwa mtu mmoja mmoja, na uwajibikaji wa kitaasisi. Lazima tuhakikishe amri ya mahakama iliyotaka sheria zirekebishwe ili kuharamisha kabisa ndoa za utotoni inatekelezwaKwa kufanya hivyo, tunahitaji juhudi za kila mmoja wetu. Tunapokutana na wanaharakati vijana wenye nia na shauku ya mabadiliko kama Festo na Maeda, tuwaunge mkono kuzitangaza kazi zao, na kutoa wito kwa kila mtanzania kutimiza jukumu lake la kulinda wasichana wetu''.*

---- Mwisho ----

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:

Annastazia Rugaba, Twaweza **e:** arugaba@twaweza.org | **t:** +255 687 222 197	Sara Bedah, Msichana Initiative **e:** sara.akwisombe@msichana.or.tz | **t:** +255 769 507 435

Maelezo kwa Wahariri

- Twaweza inafanya kazi ya kuonesha Uatayri wa wananchi kuchukua hatua, kukuza sauti za wananchi, na kulinda na kukuza nafasi ya kiraia www.twaweza.org
- Msichana inititive inafanya kazi kuboresha maisha ya wasichana wadogo kupitia kukuza fursa za kupata elimu, kuimarisha mifumo ya ulinzi wa watoto, kuwezesha upatikanaji wa vifaa bora vya usafi wa hedhi, na kuhimiza mageuzi ya kisheria na sera www.msichana.or.tz